

TANGAZO LA VYOMBO VYA HABARI

BABYLONE

MAONYESHO YA BABYLONE YANAKULETEA WASANII AMBAO HUSHUGHULIKIA MAMBO YA USEMI, asili ya utata wa kimsingi wa lugha yoyote, kutokuelewana kwa kudumu ambako ni tishio la mawasiliano na tafsiri zote, wingi wa dhana ambao neno humiliki kutoka lugha moja hadi nyingine. Mada kuu ya maonyesho haya ni lugha nyingi za kigeni, ambazo wakati mwingine husahaulika. Mada hii italenga kuonyesha matatizo na ukosefu wa usanifu wa lugha. Maonyesho ya *Babylone* husaidia wasanii ambao huunda maumbo ya maneno na maneno ya maumbo. Herufi zilizopotea, maneno mapya muhimu au "wasilisho la mawasilisho" yatatushinikiza kutoka usemi wa watoto wachanga hadi utata wa lugha, kuptia kutafakari kuhusu dhamira ya lugha.

Lugha hutuathiri kwa sababu ndiyo macho yetu ya kuutazama ulimwengu. Aina elekezi na iliyowasilishwa ya lugha, ambayo hubadilisha mtazamo, huifasili, kuiieleza na hata kuisaliti lugha. Lugha asili hubaini mtazamo wetu kwa undani zaidi. Lugha tekelezi hujumuisha kitendo wakati *kusema ni kutenda*. Lugha ya kishairi ni muhimu katika fasihi, ambayo ni lugha hujifasili kama chombo cha umaridadi. Lugha asili, pamoja na usemi na uandishi wake ni shughuli za kidesturi ambazo zimejikita katika mafumbo na hekaya kutoka jadi.

Lugha za kusemi au michoro, lugha za ishara na mifano, asili au za kubuniwa, zilizopo au zilizoangamia, rasmi au za misimbo - lugha ni nyingi sana, ingawa idadi na utofauti wake unapungua kutokana na utandawazi. Hata hivyo, maelewano hayafai kuwa ya upande mmoja, ya idhini au usanifu. Kinyume na hili, yanapaswa kushiriki hisia na fahamu mbalimbali. Kwa sababu "mipaka ya mtazamo wangu" (kama alivyosema Ludwig Wittgenstein) huwekwa na lugha yangu, ili kuyafikia inambidi mtu kujitahidi kujua mitazamo mingine yamkini. Pia inamaanisha kujitahidi "kubaini dhana muhimu za tamaduni zetu, na muhimu zaidi, dhana zinazopelekea wazo la "uhalisi" " (Roland Barthes). Kwa sababu hatuingiliani na vitu *kama vilivyo tu*, je, inamaanisha kwamba kufahamu maisha kupitia lugha ni kufamahu ulimwengu kwa njia mbadala? Au, je, inamaanisha kuwa na maono, kubadilisha na kuumba ulimwengu kama wanavyopendekeza wasanii?

Wasanii

Camille Bondon

Erik Bullo

Valery Chtak

Dora García

Valère Novarina

Charles Pennequin

Dominique Petitgand

Mladen Stilić

Afisa Mwangalizi

Nicolas Audureau

Babylone

04 Februari - 25 Machi, 2017

Ufunguzi

Ijumaa 03 Februari, 2017 - 7pm

Upatikanaji

Bila malipo

Jumanne hadi Jumamosi: 2-6pm